



TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA
Kitalu Na. 339, Mtaa wa Nyerere - Kilimani
S.L.P 1049, DODOMA
Simu: +255 22 2135747/8; 2137125; 2135222
Faksi: +255 22 2111281
Barua Pepe: info@chragg.go.tz
Tovuti: www.chragg.go.tz

Desemba 23, 2019

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Kukamatwa kwa Mfanyakazi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Tito Magoti na Wenzake

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala na Bora (THBUB) imepata taarifa kupitia vyombo vya habari za kutekwa kwa Afisa wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Bw. Tito Magoti kuanzia Ijumaa Disemba 20, 2019. Hata hivyo, baadae taarifa zilizopatikana kupitia vyombo vya habari zilimnukuu Kamanda wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam wa Jeshi la Polisi, SACP, Lazaro Mambosasa akiueleza umma kuwa Afisa huyo anashikiliwa pamoja na watu wengine watatu (3) kwa ajili ya mahojiano na uchunguzi kwa tuhuma za makosa ya jinai ambayo hayakuwekwa wazi.

Tume inatambua kuwa Jeshi la Polisi ndio chombo chenye mamlaka ya kusimamia usalama wa raia pamoja na mali zao. Hivyo, Tume inalishauri Jeshi la Polisi kushughulikia jambo hili kwa kuzingatia sheria na kuheshimu haki za binadamu wakati wote ambapo mahojiano na uchunguzi huo utakapokuwa unaendelea. Tume inaendelea kufuatilia tukio hili na kutafuta maelezo zaidi kutoka pande zote zinazohusika.

Imetolewa na:

Mohamed Khamis Hamad

Makamu Mwenyekiti

TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA

Desemba 23, 2019